# MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

## KANDA YA KATI

**TMDA**

Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

JARIDA LA MTANDAONI JANUARI - JUNI 2022




JANUARI - JUNI 2022

# YALIYOMO

03. Utangulizi kuhusu Kanda ya Kati

04. Salamu kutoka kwa Meneja wa Kanda

05. Elimu ya athari za tumbaku mtaa kwa mtaa jijini Dodoma

08. Uteketezaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi

10. Mafunzo ya wakaguzi wa dawa ngazi ya Halmashauri

13. TMDA Kanda ya Kati kutoka magazetini na mitandaoni

14. Maadhimisho ya wiki ya mazingira duniani

15. Matukio katika picha

24. Wafanyakazi Hodari

**KAMATI YA WAHARIRI;**

**Mhariri Mkuu:**
Sonia Mkumbwa

**Wahariri Wasaidizi:**
Prisca Matagi
James Ndege

**Sekretarieti:**
Prisca Matagi
James Ndege
Riziki Shemula
Zakayo Kamani



# UTANGULIZI

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)** ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya yenye jukumu la kulinda afya ya jamii dhidi ya athari zinazoweza kutokana na matumizi ya bidhaa za dawa (zikiwemo chanjo), vifaa tiba na vitendanishi. Mnamo Tarehe 30 Aprili, 2022 Mamlaka ilikabidhiwa jukumu jipya la usimamizi wa bidhaa za tumbaku na kufanya jumla ya bidhaa zinazosimamiwa na TMDA kuwa nne yaani Dawa, Vifaa Tiba, Vitendanishi pamoja na Tumbaku.

Ofisi ya Kanda ya Kati ni moja ya Kanda nane (08) za Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba zilizoko nchini na inaundwa na mikoa minne ya Dodoma, Morogoro, Singida pamoja na Iringa. Kanda hii ilianzishwa mwaka 2012 na hadi kufikia sasa ina idadi ya watumishi 29.

Majukumu yanayoratibiwa na Ofisi ya TMDA Kanda ya Kati ni pamoja na kufanya usajili wa majengo yanayozalisha, kuhifadhi na kuuza bidhaa zinazodhibitiwa, kufanya ukaguzi za bidhaa katika soko; kukusanya sampuli kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara, kudhibiti uingizaji nchini na usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi, kusimamia uteketezaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi, Ufuatiliaji wa madhara yanayohisiwa kusababiswa na matumizi dawa, vifaa tiba na vitendanishi, lakini pia kutoa elimu kwa umma juu ya bidhaa zinazodhibitiwa pamoja na matumizi sahihi ya bidhaa hizo.

**Dhima** Kulinda afya ya jamiii kuzuia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

**Dira** Kuwa Mamlaka inayoongoza barani Afrika katika kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa wote.

**Falsafa** Kutoa huduma za udhibiti katika kulinda afya ya jamii na mazingira kwa kutumia wafanyakazi wenye ujuzi na ari ya kazi.

**Misingi**
- Uwazi
- Uwajibikaji
- Kufanya kazi kwa ushirikiano
- Uadilifu
- Kuzingatia uhitaji wa mteja

# SALAM ZA MENEJA WA KANDA



**Bi. Sonia Mkumbwa**
Meneja TMDA Kanda ya Kati

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuuona Mwaka Mpya wa 2022 na nipende kuwatakia heri ya mwaka mpya kwenu nyote!

Aidha, toleo hili la kwanza, ni muendelezo wa matoleo mengine yajayo, hivyo basi napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha muweze kusoma na kupata habari mbalimbali za mambo muhimu yanayofanyika katika Kanda kupitia jukwaa hili.




# TMDA YAINGIA MITAANI DODOMA KUTOA ELIMU YA ZUIO LA MATUMIZI HOLELA YA BIDHAA ZA TUMBAKU

TMDA Kanda ya Kati, kwa nyakati tofauti imeendesha zoezi la uelimishaji na ukaguzi elekezi kwa makundi mbali mbali ya kijamii juu ya udhibiti wa bidhaa za tumbaku katika maeneo yasiyoruhusiwa kisheria katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ambapo jumla ya wadau 5,664 walifikiwa.

Zoezi hilo lilihusisha mihadhara ya wazi, vikao na wamiliki pamoja na viongozi wa maeneo husika kwa lengo la kupeana uelewa juu ya matakwa ya kisheria na kikanuni kuhusiana na udhibiti wa bidhaa za tumbaku. Maeneo yaliyofikiwa ni pamoja na Soko la Job Ndugai, Stendi kuu ya mabasi ya Nanenane, Soko la Sabasaba, Soko la Majengo, maduka madogo madogo yaliyopo barabara ya 10, ghala la sigara TCC na duka la Shoppers.

Sambamba na uelimishaji huo, maafisa kutoka TMDA walifanya ukaguzi elekezi katika maeneo hayo ya hadhara ili




*Wakaguzi wa TMDA Kanda ya Kati wakikagua baadhi ya bidhaa za tumbaku katika mojawapo ya maduka makubwa jijini Dodoma*

kuhakikisha alama za makatazo ya uvutaji holela wa bidhaa za tumbaku yanabainishwa ili kulinda afya ya jamii isiyotumia bidhaa hizo.

Zoezi hilo pia lilifanyika katika shule za sekondari zikiwapo shule za sekondari za Kikombo, Mtumba, Nala, Nkuhungu, Chigongwe, Bihawana Seminari, St. Home na nyinginezo ambazo zipo katika Halmashauri ya jiji la Dodoma ambapo pia zoezi hilo liliambatana na uanzishaji wa vilabu vya TMDA ambavyo vitasaidia kuendelea kusambaza uelewa juu ya majukumu na kazi zinazofanywa na Mamlaka.

Hadhara hizo pia zilipatiwa elimu juu ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya bidhaa za tumbaku na kuwafahamisha mikakati ambayo Serikali imeiweka katika udhibiti matumizi holela ya bidhaa za tumbaku ili kuwalinda wasiotumia bidhaa hizo pamoja na watoto walio na umri chini ya miaka 18.

Ili kuhakikisha elimu juu ya majukumu yake na udhibiti wa bidhaa za tumbaku inawafikia watu wengi katika jamii, TMDA Kanda ya Kati ilitumia vyombo vya habari mbalimbali ikiwamo redio, televisheni, magazeti, blogu pamoja na mitandao ya




Wakati huo huo, katika kuendelea kutoa uelewa juu ya jukumu jipya la udhibiti wa bidhaa za tumbaku, TMDA Kanda ya Kati imefanikiwa kufanya vikao kazi na viongozi ngazi ya mkoa, manispaa na jiji, wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wa mikoa na manispaa pamoja na viongozi wa wafanyabiashara katika mikoa mitatu kati ya minne inayosimamiwa na Kanda ya Kati ambayo ni Dodoma, Iringa na Singida.

kijamii ambapo TBC FM na TV, ITV, Channel 10, Abood FM, Abood TV, CFM Redio, AFM Redio, Nipashe, Mwananchi, Michuzi, Millard Ayo, Jamii Forum, Lemutuz na gazeti la Wamachinga walirusha habari hizo.




*Mkuu wa Mkoa wa Iringa **Bi. Queen Sendiga** (wa tatu kushoto safu ya mbele) katika picha ya pamoja na timu ya viongozi ngazi ya Mkoa na Manispaa ya Iringa pamoja na timu ya watumishi Kanda ya Kati ikingozwa na Meneja wa Kanda **Bi. Sonia Mkumbwa** wakati TMDA ilipoendesha kikao kazi na viongozi hao kilichokua na lengo la kupeana uelewa juu ya udhibiti wa bidhaa za tumbaku mkoani humo.*



Kwa kuzingatia jitihada zilizowekwa na Wizara yenye dhamana ya afya kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Kanda ya Kati inawahakikishia wananchi kuwa afya zao zitaendelea kulindwa.




# TMDA KANDA YA KATI YATEKETEZA BIDHAA ZISIZOFAA KWA MATUMIZI ZENYE THAMANI TAKRIBAN BIL 2.99

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Kati katika kutekeleza jukumu lake la kulinda afya ya jamii iliteketeza bidhaa zenye thamani ya TZS 2,995,082,583/= na uzito wa takribani Tani 21.3.

Bidhaa hizo zinajumuisha dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambavyo viliondolewa katika soko kutokana na mapungufu mbalimbali ya kutokidhi matakwa ya sheria ikiwemo kuisha muda wa matumizi, kutosajiliwa nchini pamoja na kuwa duni. Jumla hiyo inahusisha dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI (ARV-Legacy) ambapo uteketezaji wake uliratibiwa na Bohari Kuu ya Dawa Tanzania (MSD). Bidhaa hizo zilitolewa kupitia kaguzi mbalimbali zilizofanyika katika mikoa ya Dodoma, Singida, Morogoro na Iringa.

Aidha, uteketezaji pia ulifanyika kwa chupa tupu za dawa zenye asili ya kulevya zilizokuwa zimehifadhiwa kwa muda mrefu katika maeneo ya kutolea huduma za afya kutokana na wahusika kutofahamu taratibu hizo ulifanyika ambapo jumla ya chupa tupu 158,577 zenye uzito wa takribani 211.9kg zilichomwa katika matanuru yaliyopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Lumuma iliyopo Mpwapwa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa.





*Mkaguzi wa dawa wa TMDA Kanda ya Kati **Bw. Emmanuel Ndejembi** akiendelea na zoezi la uteketezaji wa bidhaa zisizofaa kwa matumizi.*

Meneja wa TMDA Kanda ya Kati, **Bi. Sonia Mkumbwa** kwa nyakati tofauti, aliwaaasa wasimamizi, wauzaji na wamiliki wa hospitali, vituo vya afya, famasi na maduka ya dawa muhimu za binadamu na mifugo kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo ili kuepuka kutoa bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi na kuwasihi kuwasilisha maombi ya uteketezaji wa hiari ili kulinda afya ya jamii. ***"TMDA itatumia rasilimali zake ili kuendelea kulinda afya ya wananchi ambao ndio msingi mkubwa katika kuchagiza maendeleo ya nchi yanayosimamiwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan"***, Meneja huyo alisisitiza.






*Washiriki wa mafunzo hayo kutoka mkoa wa Morogoro wakiwa katika picha ya pamoja na timu ya wawezeshaji kutoka TMDA Kanda ya Kati ikiongozwa na Meneja wa Kanda ya Kati* ***Bi. Sonia Mkumbwa.***

# WAKAGUZI NGAZI YA HALMASHAURI MKOANI MOROGORO WAIVA NA MAFUNZO KUTOKA TMDA

Katika kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yake Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) Kanda ya Kati, yaendesha mafunzo ya siku mbili katika mkoa wa Morogoro yaliyolenga kuwajengea uwezo wakaguzi walioteuliwa kutekeleza baadhi ya madaraka na majukumu yaliyokasimiwa kwa Mamlaka ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mujibu wa Sheria.

Walengwa wa mafunzo hayo walikuwa wafamasia, wataalamu wa maabara, madaktari wa wanadamu na mifugo katika ngazi ya Halmashauri walioteuliwa kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko vinakidhi matakwa ya ubora, usalama na ufanisi.

Katika hilo, Meneja wa TMDA Kanda ya Kati, Bi. Sonia Mkumbwa alinukuliwa akisema,

***"Kwa sababu TMDA iko Kitaifa na katika Ofisi za Kanda hivyo hatuwezi kufika kwa wakati katika kila Halmashauri pale inapohitajika kutokana na ukubwa wa maeneo ya nchi yetu. Hivyo, TMDA inaendesha mafunzo haya ili kuwajengea uwezo wataalamu hawa waliopo katika halmashauri ili waweze kutekeleza kwa ufanisi majukumu yaliyokasimiwa na pia kusogeza karibu na jamii huduma zitolewazo na TMDA..."***




*Meneja wa TMDA Kanda ya Kati **Bi. Sonia Mkumbwa** (Kulia) akitoa neno la utangulizi kwa washiriki wa mafunzo hayo. Katikati ni Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro **Bi. Rozalia Rwegasira** ambaye alikua mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo hayo.*

Akifungua mafunzo hayo, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Morogoro Dkt. Rozaria Rwegasira pamoja na kushukuru TMDA kutoa mafunzo kwa watalaamu hao aliwataka TMDA waendelee kuwajengea uwezo zaidi watalaam hao kwa kuwa Elimu haina mwisho na kwamba kadri watakavyojengewa uwezo ndivyo watakuwa na uwezo wa kudhibiti madhara makubwa kwa binadamu yatokanayo na kutumia dawa, vifaa tiba au vitendanishi visivyo na ubora.

Aidha, washiriki wa mafunzo hayo akiwemo Felisia Mapunda ambaye ni Mfamasia wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga pamoja na kuishukuru Serikali kupitia TMDA kushiriki mafunzo hayo amebainisha kuwa mafunzo hayo yatawasaidia kwenda kufanya kazi kwa weledi lakini zaidi kwenda kumlinda mwananchi kutopata dawa ambazo hazina ubora.




*Meneja wa TMDA Kanda ya Kati **Bi. Sonia Mkumbwa** (Aliyesimama) akisisitiza jambo kwa washiriki wa mafunzo wakati wa kufunga rasmi mafunzo hayo.*




*Mkaguzi wa TMDA Kanda ya Kati **Bi. Riziki Shemula** (Aliyesimama) akiwasilisha mojawapo ya mada kwa washiriki wa mafunzo hayo.*

# TMDA KANDA YA KATI KUTOKA MAGAZETINI NA MITANDAONI



Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijuakali akizungumza katika kikao kuhusu ulinzi wa maliasili mjini Sumbawanga, Rukwa.Katika mkutano huo alishauri watumishi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuhakikisha vibali vinavyotolewa kwa ajili ya uvunaji mazao ya misitu vinatumika katika maeneo yaliyokusudiwa ili kulinda maliasili za taifa. (Picha na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Rukwa).

## TMDA yabaini maabara, maduka yakiuza dawa isivyostahili

Na Magnus Mahenge, Dodoma

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imekusanya dawa zilizo halali na muda wake haujapita zenye thamani ya Sh milioni 16.6 lakini zilikuwa kwenye maduka na maabara ambazo hazistahili kuwa na dawa hizo.

Kaimu Meneja wa TMDA Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa alisema dawa hizo ni salama, isipokuwa zilikuwa kwenye maeneo yasiyotakiwa. Alizikabidhi kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk Best Magoma.

Sonia aliomba ofisi ya mganga mkuu kuhakikisha kwamba dawa hizo zilizokabidhiwa kwao, zinarudishwa kwenye mfumo.

"Dawa hizo ni bora, salama na fanisi ila hazikustahili kuwepo katika maduka ya dawa na maabara ambayo hayakutakiwa kuwa na dawa hizi," alisema.

Sonia alisema wamezirudisha kwa mganga mkuu wa mkoa ili azipangie matumizi kwenye maeneo zinapostahili kwani nyingine zinatumika baada ya maelezo ya daktari, nyingine haziingiliani na zinatakiwa kuepusha athari.

Kama dawa hizo zinawekwa maduka ya dawa maalumu au maabara kwenye halmashauri, inatakiwa awepo daktari anayeweza kushauri matumizi yake bora.

TMDA imerudisha dawa hizo kwa mganga mkuu wa mkoa kwa lengo la kuzipangia matumizi na katika maeneo na madaraja husika.

"Zimepatikana kutoka katika vyanzo sahihi isipokuwa waagizaji wamekuwa si wakweli wanaponunua kwani hawaelezi kwamba ni duka la daraja gani na maabara ni za kupima wala si kuuza dawa," alisema.

Sonia alisema wamekuwa wakifanya ukaguzi huo mara kwa mara kuhakikisha afya inakuwa salama.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Best Magoma alisema ukaguzi huo umekuwa ukifanyika katika halmashauri zote nchini.

"Inawezekana nia ya hospitali na vituo vya afya ni kutoa huduma kwa jamii, lakini kuna madaraja ya utoaji wa huduma hiyo kwani hazina wataalamu wa kueleza matumizi sahihi ya dawa hizo," alisema.

Alisema wauzaji wa dawa wanatakiwa kuheshimu taaluma hiyo kwa kuuza zinazoendana na madaraja ya vituo hivyo kwani kuziuza bila maelekezo ya wataalamu, inaweza kusababisha changamoto nyingi.

Changamoto hizo ni pamoja na kusababisha usugu, kuongeza gharama za maisha kwa kutumia fedha nyingi bila kupata tiba lakini pia ni hasara kwa nchi.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (kushoto) akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu matarajio ya mwonekano wa mahema wakati wa ziara ya kukagua mradi wa TANAPA wa ujenzi wa mahema matatu kwenye hifadhi ya Kisiwa cha Saanane, Mwanza juzi. (Na Mpiga Picha Maalumu)

## Matumizi ya tumbaku yapigwa marufuku

Na Dotto Mwaibale, Singida

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) imepiga marufuku matumizi ya bidhaa za tumbaku katika maeneo yasiyo rasmi ili kulinda afya za jamii.

Agizo hilo lilitolewa katika kikao kazi cha kutoa welewa wa udhibiti wa bidhaa za tumbaku kilichokutanisha TMDA, uongozi wa wafanyabiashara na viongozi wa ngazi ya mkoa na Manispaa ya Singida mwanzoni mwa wiki.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Kaimu Meneja wa TMDA Kanda ya Kati, Sonia Mkumbwa alisema ni jambo zuri kwa watumiaji wa bidhaa hizo, kutengewa maeneo maalumu ya matumizi ya bidhaa hizo, ili kuondoa matumizi hayo maeneo ya hadharani, ili kusaidia kulinda afya za watu ambao hawatumii tumbaku.

"Ni vizuri sasa watumiaji wa bidhaa za tumbaku (wavutaji wa sigara) kutengewa maeneo maalumu ya kutumia bidhaa hizo zitakazowekwa vibao vikavyoonesha maeneo hayo, ili iwe rahisi kutambulika badala ya hivi sasa ambapo matumizi yake yamekuwa yakifanyika hadharani," alisema Mkumbwa.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji, Lanslaus Choaji wa Mkoa wa Singida, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, wakati akifungua kikao kazi hicho, alisema mafunzo hayo ni ya muhimu sana.

Choaji aliwakaribisha na kuwashukuru wadau wote kwa kuhudhuria kikao hicho muhimu chenye lengo la kupeana welewa wa udhibiti wa matumizi ya bidhaa za tumbaku mkoani hapa, na utekelezaji wake unaofanyika nchi nzima.

"Nafahamu TMDA imekasimishwa jukumu hili la udhibiti wa matumizi ya bidhaa za tumbaku na Serikali kupitia Wizara ya Afya. Hivyo basi, nawapongeza kwa kupokea jukumu hili na bila kuchelewa, mmeandaa mpango kazi wa miaka mitatu 2021/22 hadi 2023/24). "Mpango huo ni wa utekelezaji udhibiti wa bidhaa hizi lengo likiwa ni kupunguza au kuzuia matumizi ya bidhaa za tumbaku na madhara makubwa ya kiafya, yanayoweza kusababishwa na matumizi ya bidhaa hizi," alisema Choaji.

Alisema utafiti unaonesha matumizi ya bidhaa za tumbaku yamekuwa yakiongezeka kwa kasi ulimwenguni, chimbuko lake ikiwa katika nchi zilizoendelea, lakini kwa sasa imebainika kuwa matumizi makubwa ya bidhaa hizi yako nchi zinazoendelea.

"Takwimu zimebainisha kuwa zaidi ya watu bilioni 1.3 ya watumiaji wa bidhaa za tumbaku duniani, wako katika nchi zinazoendelea.

"Aidha, utafiti umebainisha madhara makubwa yaliyoelezwa ni pamoja na vifo vya zaidi ya watu milioni 7 duniani kila mwaka vinavyosababishwa na magonjwa yanayotokana na matumizi ya bidhaa za tumbaku," alisema.

Wakati huo huo, TMDA imetoa mafunzo kwa watumishi wa afya mkoani hapa kuhusu utoaji taarifa za madhara au matukio yanayohisiwa kusabibishwa na matumizi ya dawa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo.

Akizungumza wakati akifungua mafunzo hayo, Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Mkoa ambaye alikuwa awe mgeni rasmi, Elikana Lubango alisema mafunzo hayo yatatatua changamoto ya utoaji taarifa juu ya madhara



GAZETI LA
# WAMACHINGA
SAUTI YA WANYONGE

ISSN: Toleo Na. 136 | JUMAMOSI | MACHI 19, 2022 | Bei Tsh. 500

## Chadema kugomea mkutano wa TCD


TMDA : Marufuku kuvuta sigara maeneo yasiyorasmi

Yashauri yatengwe maeneo maalumu ya wavutaji ili kulinda afya za wengine









# MAADHIMISHO YA WIKI YA MAZINGIRA DUNIANI, DODOMA

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba TMDA Kanda ya Kati mwaka huu ilishiriki katika maonyesho ya maadhimisho ya Wiki ya Mazingira Duniani katika viwanja vya ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete ambapo Mgeni Rasmi katika siku ya uzinduzi wa maadhimisho hayo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Anthony Mtaka ambaye alitembelea banda la TMDA na kupongeza utendaji kazi wa Mamlaka hiyo.




Katika maonyesho hayo TMDA Kanda ya Kati ilipata wasaa wa kueleza miongozo mbalimbali kuhusu udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi huku vipeperushi vya mamlaka hiyo vikigawiwa kwa washiriki na wageni waliotembelea banda la maonyesho kwa lengo la kusogeza elimu zaidi kwa wananchi juu ya majukumu na kazi za TMDA.



Jumla ya wadau 308 walitembelea banda la TMDA ikiwa ni pamoja na makundi ya wanafunzi/wanachuo, wajasiriamali, wadau na wananchi waliopatiwa elimu na kutoa maoni yao Ili kuboresha utendaji kazi wa TMDA, ikiwa ni pamoja na kuiomba Mamlaka kuandaa sinema na kupita na gari la matangazo katika maeneo ya hadhara yenye watu wengi kama vile minada na pia kuweka stika zinazoonesha uvutaji sigara hauruhusiwi katika maeneo mbalimbali ya kijamii kama maduka, masoko, maeneo ya chakula kwenye baa pamoja na sehemu za starehe.



Maoni mengine yaliyotolewa na baadhi ya wadau hao ni kuiomba TMDA iwe inaandaa na kutumia vifaa vidogo vidogo vya matangazo wakati wa maonesho, kufuatilia kwa karibu usalama wa dawa za vijiua sumu (antibiotics) za mifugo ili kuhakikisha zile zenye ubora ndio zinapatikana katika soko lakini pia TMDA na kuimarisha klabu zake za shule za sekondari ilizozianzisha wakati wa TFDA kwani ufanisi wake kwa sasa umepungua sana.

Maadhimisho hayo ya wiki ya mazingira duniani huadhimishwa kuanzia kuanzia tarehe 01 hadi 05 kila mwaka ambapo Mwaka huu yakiwa chini ya kauli mbiu ya ***"Tanzania ni Moja, Tunza Mazingira"*** yalihitimishwa Juni tano na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Wa Tanzania Mhe. Kasim Majaliwa.

# MATUKIO KATIKA PICHA







*Watumishi wa TMDA Kanda ya Kati waungana na wafanyakazi wengine wote duniani katika shamra shamra za maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniania ambayo kwa mwaka 2022 yaliyofanyika kitaifa katika uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma.* ***Kauli mbiu katika maadhimisho hayo ilikua "Mishahara na Maslahi Bora Kwa wafanyakazi Ndiyo Kilio Chetu: Kazi Iendelee".***

# MATUKIO KATIKA PICHA







*Meneja wa Kanda ya Kati* ***Bi. Sonia Mkumbwa*** *akikabidhi taulo za kike za kutumia na kutupa (Disposable Sanitary Pads) zenye thamani ya shilingi milioni mbili (Tsh. 2,000,000/=) kwa kiongozi wa Chama cha Wanafunzi Wafamasia Tanzania kutoka Chuo Kikuu cha St. John (TAPSA-SJUT)* ***Bw. Joseph E. Mkude*** *kilichopo katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma mkoani Dodoma kwa lengo la kutolewa kama msaada katika vituo vya kulelea watoto yatima vilivyopo jijini Dodoma wakati chama hicho kilipoendesha kampeni ya elimu juu ya hedhi salama jijini humo.*







*Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Bwana* ***Best Magoma*** *(wa pili kushoto) akipokea kasha la dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 16 kutoka kwa Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Kati* ***Bi. Sonia Mkumbwa.*** *Bidhaa hizo ni zile zilizokamatwa na TMDA Mkoani Dodoma kwenye Maduka ya Dawa Muhimu wakati wa operesheni maalum iliyoendeshwa na TMDA ili kuwabaini wauzaji wa dawa wenye leseni zisizoruhusu kuuzwa kwa dawa hizo kwenye maduka yao. Dawa na vifaa tiba hivyo bado zinafaa kwa matumizi ya Binadamu na zitagawanywa kwenye Hospitali na vituo vya afya vyenye uhitaji.*

# MATUKIO KATIKA PICHA








*Watumishi wa TMDA Kanda ya Kati wafanya hafla fupi ya kumpongeza **Bi. Sonia Mkumbwa** kwa kuthibitishwa kuwa meneja Kanda ya Kati. Kongole MENEJA KANDA YA KATI.*

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Meneja wa TMDA sehemu ya Mipango na Tathmini* ***Bw. Damas Matiku*** *akipokea tuzo ya shukrani kutoka kwa Katibu Mkuu Utumishi* ***Dkt. Laurean Ndumbaro*** *wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Tathmini na Ufuatiliaji yaliyofanyika jijini Dodoma.*




*Mkaguzi wa Dawa wa Kanda* ***Bi. Riziki Shemula*** *akitoa elimu juu ya majukumu ya TMDA kwa baadhi ya wadau waliotembelea banda la TMDA wakati wa maadhimisho ya wiki ya Tathmini na Ufuatiliaji yaliyofanyika jijini Dodoma.*

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Mkutubi Mwandamizi **Bw. James Ndege** akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mkuu wa TMDA **Bw. Adam Fimbo** kuhusu uanzishwaji wa Maktaba mpya katika ofisi ya TMDA Kanda ya Kati - Dodoma.*




*Meneja wa TMDA Kanda ya Kati **Bi. Sonia Mkumbwa** akiwa katika picha ya pamoja na Mkuu wa wilaya wa Dodoma, Viongozi ngazi ya Mkoa, watumishi wa Halmashauri ya Jiji, viongozi wa wafanyabiashara pamoja na wakuu wa vyombo vya Ulinzi na Usalama wa mkoa wa Dodoma mara tu baada ya kumaliza kikao kazi cha kupeana uelewa juu ya udhibiti wa bidhaa za tumbaku.*

# MATUKIO KATIKA PICHA










*Wanawake wa TMDA Kanda ya Kati waungana na wanawake wengine wote duniani kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani tarehe 08 Machi, 2022.* ***Kauli mbiu ya maadhimisho hayo ilikua,, " Kizazi cha Usawa Kwa Maendeleo Endelevu"***

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Mkaguzi wa Dawa wa Kanda **Bi. Riziki Shemula** akitoa elimu juu ya majukumu mbalimbali yafanywayo na TMDA kwa baadhi ya wadau waliotembelea banda la TMDA wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Ufuatiliaji na na Tathmini yaliyofanyika katika ukumbi wa LAPF jijini Dodoma.*



*Hafla fupi ya kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa mkaguzi wa Dawa wa Kanda **Bw. Zakayo Kamani** iliyoandaliwa na watumishi wenzie wa Kanda ya Kati*

# MATUKIO KATIKA PICHA





*Watumishi wa TMDA Kanda ya Kati waandaa hafla fupi ya kumuaga na kumtakia kila la kheri* ***Bw. Hussein Makame*** *aliyehamishwa kutoka Kanda ya Kati na kwenda Kanda ya Kusini.*

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Watumishi wa TMDA Kanda ya Kati wakiwa katika picha ya pamoja na meneja wa Kanda **Bi. Sonia Mkumbwa** (Safu ya mbele katikati).*




*Watumishi wa TMDA Kanda ya Kati wakiwa katika picha ya pamoja ya ukumbusho ya watumishi wa TMDA pamoja na mfanyakazi hodari wa Kanda wa robo ya nne ya mwaka 2021/2022 **Bi. Mwasiti Mfutakamba** (Safu ya mbele kushoto), Katikati ni Kaimu Meneja wa Kanda **Bw. Zakayo Kamani** na kulia ni mshindi wa pili katika uchaguzi huo **Bw. Mohammed Iwoodya***

# WAFANYAKAZI HODARI




*Mfanyakazi Hodari wa TMDA Kanda ya Kati kwa kipindi cha Robo ya Nne ya Mwaka 2021/ 2022. **Bi. Mwasiti Mfutakamba***




*Mfanyakazi hodari wa Kanda kwa mwaka wa Fedha 2021/ 2022 **Bi. Riziki Shemula***




# “TMDA Hulinda Afya ya Jamii”

TMDA

Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**
Kanda ya Kati
S.L.P 1253 Dodoma.
Simu: +255 26 2320156
Barua pepe: info.dodoma@tmda.go.tz

@tmda tanzania